# MINONG'ONO GIZANI

## ABUBAKAR NKUNDWASON

©MWANDISHI
Abubakar Nkundwason
Chapisho la kwanza; Oktoba, 2025.

**ISBN 978-9976-5028-0-6**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inaruhusiwa kuhamishwa kwa namna yoyote ile, iwe ya kimaandishi au kielektroniki bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Kukiukwa kwa agizo hili ni uvunjwaji wa sheria.

Msanifu kurasa: Evona Dastan
Mhariri: Joe Lwebagaramu.

**Wasiliniana nami:**
WhatsApp: +255 753 905 099
Simu ya mkononi: +255 753 905 099.
Mbeya, Tanzania.

Kimechapishwa na: *SIA Connection.*
Dar es Salaam.

**ILANI:** Pamoja na kwamba, visa vinavyopatikana kwenye riwaya hii vimechochewa na matukio halisi yanayotukia kwenye jamii zetu kila kukicha; mfano: ukiukwaji wa haki na sheria, n.k. Hata hivyo, simulizi ya kitabu hiki ni ya kubuni na haimuhusu mtu yeyote yule moja kwa moja.

*Mara nyingi sheria huwa kipofu si kwa haki, bali kwa ukweli.*
*Na pale udhalimu unapovaa joho la mahakama, hata wauaji hujificha nyuma ya vifungu vya sheria, huku waathirika wakihukumiwa kwa kimya chao.*

**Abubakar Nkundwason**
*Septemba, 2025.*
*Mbeya, Tanzania.*

**VITABU VINGINE VYA ABUBAKAR NKUNDWASON**

*1. Oparesheni Khartoim 01*
*2. Oparesheni Khartoum 01*
*(Kufa Ama Kupona).*

## SHUKURANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uweza na rehema zake hata kunijalia kipaji cha kufikisha mawazo yangu kwa jamii yangu na dunia kwa ujumla, kwa namna hii ya utunzi wa riiwaya. Hakika hii ni neema ya ajabu na siwezi kuipuuza.

Shukurani zangu za dhati pia ni kwa mama yangu mzazi Hamida Mussa, mke wangu Sunaiya Sandali Chowo, watoto wangu Sameer, Farheen, Adady na Amir. Hakika familia yangu hii imekuwa na mimi katika kila hatua ya maisha yangu - na kila mara ninaiona nguvu mpya pale ninapoona watu wangu wapo na mimi kwenye kila jambo.

Aidha, nachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote, ambao kwa namna moja ama nyingine wamechangia kufanikisha kutoka kwa kitabu hiki. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

## SURA YA KWANZA

*Dar es Salaam, Tanzania*

Ni mchana tayari.

Wengine hawakuamini.

*"Hee! Saa mbona zinakimbia namna hii?"*

Ilishitua!

Kumekucha punde na watu bado wanahisi ni asubuhi — maana hata kifungua kinywa walichopata hakijatulia tumboni.

Kufumba na kufumbua saa zimesonga mbele hadi katikati ya siku na ndicho hicho kinachowaacha watu midomo wazi. Kwa hakika, saa hazikawii. Zinakimbia kwa mwendo wa upepo — mwendo wa kujibalaguza, kujitupa tupa na wakati mwingine mwendo wa bila mpangilio lakini wenye kasi ya ajabu. Na kwa kasi hiyo, huta kosea ukiuita mwendo wa umeme: *shwaa!* Siku zimepita! Kukapua tu, siku imekwenda. Hujakaa sawa, wiki imepita; kisha mwezi, mwaka, halafu unashangaa unaaga watu unaowafahamu!

Huyu kaondoka na yule amekwenda — kama siku na majira ya mwaka vinavyopita. Sasa unagundua; kumbe siku za maisha si

kitu kabisa. Kwa yote tuliyoyaona na kuyasikia; yakija na kupita na siku zake, ni kipi hata tuseme tutajivuna nacho kwamba kitadumu? Ni uhai? Ni mali? Ni biashara ama kazi za taaluma zetu? Au ni jamaa na ndugu zetu tunaowapenda? Ni kipi haswa?

Kwa hakika, ukifikiria kwa akili pevu, hakuna cha kujivuna kwenye uso huu wa dunia. Kila kitu tunachokiona au kukifurahia ni cha muda tu; mfano wa majira yanayokuja na kuondoka. Vitu vyote vipendezavyo na vichukizavyo hapa duniani ni vya kupita tu! Hata milima, bahari, na dunia yenyewe — hakuna kitakachosalia!

Basi, katika majira hayo ya mchana, kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na Bibi Titi Mohamed, palikuwa na mwanaume mrefu, mweusi, wa miraba minne. Mwanaume huyo, alikuwa na tumbo kubwa lililolalia juu ya mkanda wake wa rangi ya kahawai na alikuwa amevaa mavazi meupe, viatu vyeusi vya kung'aa, na kofia nyeusi ya plastiki. Muonekano wake uliashiria wazi kuwa ni askari wa usalama barabarani.

"Mh!" Dereva mmoja aliguna akimwona, alipokuwa akipita kwa gari. Akamwambia mwenzake:

"Oya, umemuona yule trafiki? Njemba imekwenda hewani! Utadhani vile vijitu vya kale — uzao wa mwanadamu na malaika."

Mwenzake aligeuza shingo na kumkazia macho yule trafiki. Akitikisa kichwa kwa mshangao, akasema:

"Nilishasikia stori ya mtu kama huyu kule Mwanza. Jamaa eti anachinja mbuzi mwenyewe. Anamkanyaga miguu kwa miguu yake halafu anashika shingo na kumchinja."

"Aaah! Ushaanza kuniokota sasa, mwanawane. Usipewe lifti! Unapiga mpaka honi!"

Dereva alitikisa kichwa kwa namna ya utani. "Yaani wewe, hizo stori sijui huzitoa wapi." Alisema kwa sauti ya kucheka, maana alimfahamu rafiki yake. Mjanja kweli kweli. Mtu wa Kamba. Walio karibu naye humuita *'mzee wa kuwatengeneza!'*

"Hahaha! Wewe unaona ni stori tu. Maisha halisi hayo, mzee wangu. Duniani kuna watu..."

Waliendelea kucheka, huku safari ikiendelea na mazungumzo yao yakizaa mada nyingine.

Saa ilikuwa karibu sita mchana. Jua lilikuwa likielekea katikati ya anga. Kipindi hiki, barabara nyingi za Dar es Salaam huwa na unafuu wa foleni. Ndio maana, palipokuwa na taa za usalama barabarani kama pale makutano, ilishangaza kuona trafiki akiwa bado anaongoza vyombo vya moto na wapita njia.

Haikujulikana mara moja kwa nini alikuwa akifanya hivyo. Baadhi ya madereva walidhani huenda kulikuwa na msafara unaotarajiwa kupita, lakini haikuwa hivyo. Namna alivyoyaongoza magari, pikipiki, na watu, haikuashiria kufungua njia.

Pamoja na maswali mengi, hakuna aliyemkaribia kumuuliza chochote. Kila mtu alitii sheria bila shuruti.

Wakati huyo trafiki akiendelea kuongoza magari, takribani mita mia mbili kutoka pale — kuelekea Hoteli ya Peacock — alikuwepo mwanaume mwingine aliyevuta hisia za wapita njia. Mwanaume huyu alionekana nusu mwendawazimu, nusu timamu.

Kilichomfanya aonekane kama mwendawazimu ni mavazi na nywele zake. Alivaa tisheti chakavu yenye nembo ya chama cha zamani cha siasa — *Tanzania Labour Party (TLP)* — iliyofifia na kuchanika matobo kadhaa. Chini, alivaa kaptura ya *jeans* iliyokatwa kwa kifaa butu, ikafumuka ovyo. Nywele zake zilikuwa zimenenepa na kutimka ovyo. Ndevu zake zilikuwa zimekua kiholela, kana kwamba ni majani yaliyoota jalalani. Mavazi yake yalikuwa machafu sana. Miguuni, alivaa kandambili nyekundu zilizotoboka kwenye visigino.

Lakini tabia yake haikulingana na mwonekano wake. Hakuwa na tabia za kawaida za wendawazimu wa mitaani — kuzungumza peke yao au kuokota vitu ovyo. Badala yake, alisimama kwa utulivu, huku akiwatazama wapita njia kwa macho ya mtu mwenye akili timamu. Alikuwa kando ya nguzo ya taa za barabarani, akiwa amebeba furushi kubwa lililopitishwa begani, mkono wa kulia ukilishikilia kwa nguvu.

Watu walipita, maisha yaliendelea kama kawaida.

Lakini ghafla — kama radi ya ghafla — risasi zilirindima kutoka eneo la Hoteli ya Peacock.

Kwanza, hazikuwashitua watu sana. Wengi walidhani ni baruti.

“Oya, sikia hiyo! Mashine hiyo!” mmoja alisema akimweleza mwenzake.

Mwingine akapinga, “Ah, wapi! Wewe unazijua mashine? Baruti hizo. Labda Wahindi wanafurahia. Si unawajua?”

Lakini, kabla yule mwingine hajapata kauli ya kumweleza

mwenziye, risasi zikarindima tena kwa nguvu zaidi. *PAA! PAA! PAA!*

Ndipo watu wakashituka.

Tafrani ikazuka.

Watu wakaanza kukimbia ovyo, wengine kupiga mayowe ya hofu, wakisaka mahali pa kujificha.

Dakika chache baadaye, gari aina ya Toyota Noah liliibuka kwa kasi kutoka ndani ya Hoteli ya Peacock. Likafunga breki ghafla mbele ya yule mwanaume aliyedhaniwa ni mwendawazimu. Mlango ukafunguliwa, naye akachoma ndani kwa ustadi wa kijeshi Pamoja na furushi lake.

Kisha gari likakimbilia kwenye makutano ya barabara. Bila kupoteza wasaa, yule trafiki naye akarukia ndani kwa ushupavu wa hali ya juu — mlango ukafungwa — na Noah ikashika njia ya Barabara ya Morogoro kwa kasi ya kutisha. Baada ya hofu, wale watu walivyopotea katika maeneo hayo, gumzo lilishika hatamu, kila mmoja akilizungumzia tukio hilo kadiri alivyowaza kichwani mwake!

Kwa waliokuwa ndani ya hoteli ya Peackock, macho yao yalishuhudia mengi zaidi ya milio ya risasi. Tukio lile lilikuwa la kutisha. Kelele za mayowe zililipuka kila kona. Watu walikimbilia chochote kilichoonekana salama — nyuma ya magari, chini ya meza, au hata nyuma ya visingiti vya maua. Alimradi zilikuwa ni hekaheka za kuokoa uhai!

Kwenye lango la mbele la Hoteli ya Peacock — ambapo

kawaida walinzi hukaa — hapakuonekana mlinzi yeyote. Walinzi nao waliungana na raia kuokoa roho zao. Hakika hofu ilitamalaki. Watu walikimbia ovyo, walipigana vikumbo, wengine wakijikwaa na kudondokea barabarani.

Tafrani ilikuwa kubwa usipime!

WAKATI gari ya wagonjwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili ilipofika hotelini hapo, tayari dakika kumi na nane zilikuwa zimepita tangu mfanyabiashara maarufu jijini Dar es Salaam, Leonard Mjifa Gabunzi, apigwe risasi na watu wasiojulikana.

Gabunzi alikuwa katika hali mbaya sana. Damu zilikuwa zikimtoka kama maji kwenye bomba, hasa kwenye maeneo aliyopigwa risasi. Kifua chake kilikuwa kimetapakaa damu.

Wauguzi wanne waliokuwa wameambatana na dereva wa ambulance walishirikiana na wasamaria wema waliokuwepo eneo la tukio kumuingiza Gabunzi ndani ya gari. Mara baada ya kuingizwa, alianza kupatiwa huduma ya dharura, na gari liliondoshwa katika eneo hilo ili kumkimbiza hospitalini Muhimbili.

Punde tu baada ya gari la wagonjwa kuondoka, liliwasili gari la polisi aina ya Toyota Land Cruiser Prado VXR, likiwa limebeba askari waliokuwa kwenye doria, wakiwa na silaha. Gari hilo lilifuatwa na Toyota Mark X, iliyowabeba makachero wawili wa Jeshi la Polisi: Inspekta Thomas Nyalandu na Sajenti Rehema Mwampamba.

Walipofika, taratibu za kipolisi zilianza kuchukuliwa mara moja.

Eneo la tukio lilizingirwa kwa utepe wa njano kuzuia mwingiliano wa watu. Makachero hao walianza uchunguzi wao kwa kupiga picha, kuchukua video kutoka kamera za *CCTV,* na kuzungumza na mashuhuda wachache.

Baada ya hapo, walielekea Hospitali ya Taifa Muhimbili, lakini walipofika, hawakuweza kumuona majeruhi, kwani alikuwa kwenye chumba cha upasuaji chini ya uangalizi mkali wa madaktari bingwa.

*****

"Tukio hili lina harufu ya kisasi," Sajenti Rehema alisema, akiangalia picha za kamera za usalama.

"Kwa nini unasema hivyo?" aliuliza Inspekta Nyalandu, akimtazama moja kwa moja.

"Angalia video hizi vizuri. Mfuatilie mshambuliaji. Mtazame toka anashuka kwenye gari; angalia anavyokwenda – ni wazi akili na mawazo yake yapo kwenye kile alichokiendea mahali hapo. Tazama, anakwenda moja kwa moja mpaka alipokuwa mhusika na kumpiga risasi halafu anaondoka bila kuchukua chochote kile. Kwa mwenendo mzima wa tukio, nina thubutu kusema huu sio wizi, bali ni shabaha ya maisha ya Gabunzi tu!"

Inspekta Nyalandu alifinya macho kwa umakini, akitazama zile picha mara mbili. Kisha akasema kwa sauti ya kutafakari:

"Una hoja."

Sajenti Rehema alimtazama bila kusema, kana kwamba hakuridhika na jibu la Inspekta. Kisha, Inspekta akasema:

“Lakini, kisasi kutoka kwa nani? Gabunzi alikuwa mmoja wa wafanyabiashara wachache wanaohusishwa na hofu ya Mungu. Alikuwa anajitolea sana—kanisani, kwenye mikutano ya injili, na kwa jamii kwa ujumla. Huo uhasama unatoka wapi?”

Sajenti Rehema alitikisa kichwa:

“Inspekta, hakuna binadamu anayeweza kutajwa kuwa mtakatifu kuliko manabii wa Mungu. Lakini hata manabii waliuawa. Sio suala la kumcha Mungu tu—maslahi ni maslahi. Kwenye maslahi ya watu, haijalishi wewe ni nani. Watafuta njia ya kukuondoa. Na pia, nani ajuaye yaliyo nyuma ya pazia? Pengine tunachokiona si tabia halisi. Maandiko yanasema: ‘Yaliyomo ndani ya moyo wa Mungu, ni bayana kwa Roho wake; na ndani ya mwanadamu, yapo bayana kwake mwenyewe.’”

Inspekta aliguna kidogo:

“Mama wa maandiko, eh?” Akatulia.

Rehema alivuta mafua asiyokuwa nayo, kama njia ya kujiandaa kusema jambo alilokuwa analifikiria.

“Naamini kabisa, mfanyabiashara mkubwa kama huyu hawezi kukosa mahasimu. Kuna mengi tutajua mbele ya safari.”

Inspekta Nyalandu alikaa kimya, akiwa amezama katika fikra zake. Alichambua kauli za Sajenti Rehema, akilinganisha na kile anachokifahamu binafsi.

Kwa hakika, Inspekta Thomas Nyalandu ni mtu wa nidhamu na umakini mkubwa. Ni mwenyeji wa mkoa wa Arusha na umri wake ni miaka 38. Kachero huyo, alijijengea heshima katika jeshi

hilo kutokana na uwezo wake mkubwa wa kushughulikia mauaji na uhalifu wa kutumia nguvu. Anafanya kazi kwa karibu na Sajenti Rehema Mwampamba, mwenyeji wa Mbeya, mwenye miaka 35. Wameshirikiana kwa zaidi ya miaka mitatu. Pamoja na kwamba, mara nyingi wanatofautiana kimtazamo, wanaheshimiana sana.

"Umekaa kimya, Inspekta."

"Natafakari, Sajenti."

"Nini hasa?"

"Kila ulichokisema na kila ninachokifahamu."

Kimya kifupi kilitawala. Kisha Sajenti Rehema akaibuka tena kwa sauti ya kushuku:

"Halafu... si huyu bwana alitangaza nia ya kugombea ubunge hivi karibuni?"

Inspekta alitazama moja kwa moja:

"Ndiyo, nakumbuka."

"Huwezi kuona kuwa hilo linaweza kuwa sababu?"

"Unamaanisha nini? Kwamba Kivanda ameamua kumuangamiza?"

"Kuna uwezekano. Habari za Kivanda si ngeni. Ametajwa kwenye visa vingi vya kuwatishia au kuwaondoa wapinzani wake, pia ni tishio kubwa kwenye biashara ya madini huko Mbeya."

Inspekta alimeza mate taratibu. Mohamed Kivanda, Mbunge wa Mbeya Mjini, alikuwa mtu anayemfahamu vizuri. Anazungumzwa

kama mtu hatari—mafia halisi. Hata ushindi wake wa ubunge ulihusishwa na mbinu zisizo za kawaida.

“Nakubaliana na wewe. Inawezekana kweli amemuona Gabunzi kama tishio.” Inspekta alisema. “Gabunzi alikuwa amejikita sana huko Mbeya. Alikuwa mdhamini mkuu wa timu ya Mpira ya Mbeya City, amesaidia mashule, na ana SACCOs zinazosaidia wafanyabiashara wadogo kwa riba ndogo. Tabaka la chini lilimpenda sana.”

“Sasa umenielewa.” Sajenti alitabasamu kidogo.

Simu ya Inspekta Nyalandu mara iliita. Alitazama jina la mpigaji:

Kopro Salumu Kidaso, maarufu kama Kopro Ninja, mmoja wa askari waliobaki Muhimbili kwa ulinzi.

“Sema Ninja.”

“Ah bosi, mambo yameharibika.”

“Kivipi?”

“Jamaa amegoma kula.”

“Leonard Gabunzi amefariki?”

“Hatunaye tena. Dakika tatu zilizopita, mwili wake wameuhamishia mochwari.”

Inspekta alishusha pumzi ndefu na kukata simu.

“Vipi?” Sajenti aliuliza kwa wasiwasi.

“Gabunzi amefariki dunia.”

"Hee!"

"Kopro Ninja kasema tayari yuko mochwari."

"Mungu wangu!" Sajenti aliguna kwa huzuni. "Kweli maisha ni mafupi mno. Hatimaye huyu naye ameondoka. Duh!"

Inspekta Nyalandu aliinua uso na kumtazama yule mwanadada mbele yake aliyekuwa anasikitika kwa msiba ule kana kwamba ulikuwa ni wa mtu wake wa karibu. Alijikuta anapata utashi wa kumuuliza: "Mbona unasikitika sana, Sajenti?"

Naye alimjibu: "Inspekta, kazi yetu inatufanya kuona vifo kila siku, lakini hii si hali ya kawaida. Vifo vinavyotokana na uhalifu havipaswi kuzoeleka. Tunapoteza kila mara watu wazuri kwa mikono ya wachache wenye tamaa na chuki."

"Ndivyo dunia ilivyo— ni uwanja wa fujo."

"Sivyo inavyopaswa kuwa. Dunia iliumbwa kuwa salama. Lakini binadamu tumekengeuka. Na sisi tulioko mstari wa mbele kusimamia sheria, ni lazima tupambane kweli. Hata kama hatuwezi kumaliza uhalifu, basi wakiingia kwenye anga zetu— wakutane na cha mtema kuni!"

*****

Sajenti Rehema ni mwanadada mwenye huruma isiyo na mfano. Wengine humuita "Mama Huruma." Anapenda haki, na mara kadhaa amewahi kuwaokoa watu waliodhulumiwa haki zao, hata kwa kuwadhamini kutoka rumande. Wengine huamini huruma yake ndiyo inamchelewesha kimaisha, lakini yeye huamini kuwa hakuna mtu anayepungukiwa kwa kusaidia wengine.

Amezaliwa katika familia ya Kiislamu, na japo wazazi wake hawakuwa wa msimamo mkali kidini, aliweza kushikamana na dini yake kwa sababu ya mafunzo ya madrasa aliyopitia utotoni.

*****

"Twende hospitalini kwa ajili ya postmotum," hatimaye Inspekta alimweleza.

"Twende'zetu!" alijibu Sajenti.

Bila kupoteza muda, walitoka ofisini, wakaelekea kwenye eneo la maegesho, wakaingia kwenye Toyota Mark X, na safari ya kuelekea Hospitali ya Taifa Muhimbili ilianza mara moja.

## SURA YA PILI

Kifo ni mgeni wa kila nyumba — hakibagui lango wala paa, wala hakina mipaka.

Iwe ni katika mastakimu ya mkwasi au kwenye kibanda cha hawinde, ipo siku kitabisha hodi.

Na siku yake hiyo, huja upesi mno; haikawii. Utajikuta ukiwaza: *"Mbona siku zote ni kama nilikuwa naishi kwenye siku hiyo hiyo!"* Na ipitapo hiyo siku, hakisahau — kwa majira na nyakati zake hurejea tena, pasipo huruma.

Kifo hakijali ikiwa waja walimudu au walishindwa kuukabili ugeni wake wa awali.

Kinachojali, ni kuitimiza desturi yake — kama mapambazuko na machweo, yasivyokoma kwenda na kurejea, ndivyo kifo kiwekavyo bidii!

Hata hivyo, pamoja na kwamba, kifo ni desturi ya dunia, kinapomchukua mchanga wa umri ama tegemezi wa familia, jamii ama taifa; basi dunia huonekana kupoteza mizani – inakuwa ni kana kwamba, tunda lililopaswa kukomaa limeanguka kabla ya wakati wake wa kuwiva! Hapo huzuni huwa mara mbili; watu humlilia marehemu kwa maumivu aliyoyaacha nyuma na humlilia